| **Sosiaalipalvelut**<br>Sosiaalipalvelut ovat kunnan palveluja, joka edistävät kunnan asukkaiden hyvinvointia ja tukevat ihmisiä haastavissa elämäntilanteissa. Sosiaalipalveluista saa apua ja neuvoja esimerkiksi silloin, jos perheessä on vammainen henkilö, perheessä tapahtuu äkillinen kriisi, tai jos henkilö on juuri muuttanut Suomeen toisesta maasta. | **Huduma za kijamii (service social)**<br>Huduma za kijamii ni huduma za manispaa za kuchangia hali njema kwa wakaaji wa manispaa na kuwasaidia watu kukabiliana (kupambana) na hali ngumu za kimaisha. Misaada na ushauri hupatikana kutoka huduma za kijamii, kwa mfano kama kuna mtu mlemavu kwenye familia, familia ikipata matatizo ghafla, ao mtu akiwa amehamia Finlande hivi karibuni kutoka nchi nyingine. |
| **Aikuissosiaalityö**<br>Aikuissosiaalityö tukee aikuisia elämässä silloin, kun heillä on vaikeuksia. Vaikeudet voivat olla haasteita asumisessa, omien asioiden hoitamisessa tai toimeentulossa. Aikuissosiaalityö on osa sosiaalipalveluja. | **Kazi za kijamii kwa watu wakubwa**<br>Kazi za kijamii kwa watu wakubwa zinawasaidia wanapokuwa na matatizo katika maisha yao. Matatizo yanaweza kutokea kuhusu makao, kushughulikia mambo yao ya kibinafsi ao mapato. Kazi za kijamii kwa watu wakubwa ni sehemu ya huduma (services) za kijamii. |

| | |
|---|---|
| **Maahanmuuttajapalvelut**<br>Maahanmuuttajapalveluissa autetaan ja neuvotaan vasta Suomeen muuttaneita asumisessa, omien asioiden hoitamisessa ja toimentuloon liittyvissä asioissa. Maahanmuuttajapalvelut voivat olla osana sosiaalipalveluja. | **Huduma za wahamiaji**<br>Katika huduma (services) za wahamiaji kuna kuwasaidia na kuwashauri wahamiaji ambao wamefika siku za karibuni inchini Finlande, katika mambo ya ukaaji mu nyumba, katika kuendesha mambo yao na mambo yanayohusiana na pesa. Huduma za wahamiaji zinawezakuwa sehemu ya huduma za kijamii. |
| **Kansaneläkelaitos = Kela**<br>Kansaneläkelaitos eli Kela on Suomen valtion laitos, jonka tehtävä on huolehtia sosiaaliturvan maksamisesta Suomessa asuville heidän eri elämän tilanteissaan. Kelan hoitamaan sosiaaliturvaan kuuluu esimerkiksi erilaisia rahallisia tukia, eli etuuksia. Kelan maksamia etuuksia ovat esimerkiksi lapsilisä ja asumistuki. | **Shirika la taifa la hifadhi ya jamii (institut Finlandais de la sécurité sociale) = Kela**<br>Shirika la taifa la hifadhi ya jamii ni taasisi (institution) ya serikali ya nchi ya Finlande. Kazi yake ni kuhusika na misaada tofauti ya kipesa ya wakaaji wa Finlande katika hali tofauti za maisha. Kela inahusika kwa mfano na misaada tofauti ya kipesa yaani mafao. Misaada inayolipwa na Kela ni kwa mfano posho ya watoto na posho ya makao (malipo ya nyumba). |
| **Etuus**<br>Etuus on rahallinen tuki jota maksaa esimerkiksi Kela. Etuuden tarkoitus on auttaa sinua taloudellisesti. Etuuksia on erilaisia eri elämäntilanteisiin. Jokaisen etuuden myöntämiseen on eri perusteet. Etuudet jaetaan ensisijaisiin ja toissijaisiin etuuksiin. | **Mafao / musaada**<br>Mafao ni musaada wa kipesa unaolipwa kwa mfano na Kela. Mafao ni kwa ajili ya kukusaidia kipesa. Mafao yanatofautiana kulingana na hali mbalimbali za maisha. Kila mafao yanakuwa na sababu tofauti za kutolewa kwake. Kuna mafao ya msingi (assistance de besoin primaire) na kuna mafao ya mwisho (assistance de dernier besoin ). |
| **Ensisijainen- ja viimesijainen etuus**<br>Ensisijaisella etuudella tarkoitetaan kaikkia muita etuuksia paitsi toimeentulotukea. Toimeentulotuki on viimesijainen etuus. Ennen toimeentulotuen hakemista sinun on täytynyt hakea muut etuudet, eli ensisijaiset etuudet. Jos siltikään tulosi, varasi ja saamasi ensisijaiset etuudet eivät riitä välttämättömiin jokapaiväisiin menoihin, voit hakea toimeentulotukea. | **Mafao ya msingi na mafao ya mwisho**<br>Mafao ya msingi yanamaanisha misaada yote mingine isipokuwa posho ya matumizi ya kimsingi (posho ya kujikimu). Posho ya matumizi ya kimsingi ni mafao ya mwisho yanyoweza kupatikana. Mbele ya kuomba posho ya matumizi ya kimsingi unapashwa kuwa umeomba kwanza mafao mengine, yaani mafao ya msingi. Na kama bado mapato, makuta yako na mafao ya msingi uliyopata hayaenezi matumizi yako ya kila siku ambayo ni ya muhimu, unaweza kuomba posho ya matumizi ya kimsingi. |
| **Vammaisetuus**<br>Vammaisetuutta maksetaan vammaiselle tai pitkäaikaisesti sairaalle henkilölle, jotta hän selviytyisi paremmin jokapäiväisessä elämässä. | **Mafao wa ulemavu**<br>Mafao wa ulemavu ni musaada unaopewa kwa mlemavu ao mgonjwa wa muda mrefu, ili apate kuendesha vizuri maisha ya kila siku. |
| **Takuueläke**<br>Takuueläke on etuus, jota maksetaan eläkkeen saajalle, joka ei saa mitään muuta eläkettä tai eläkkeen määrä on pieni. | **Dhamana ya pensheni (garantie de la pension)**<br>Dhamana ya pensheni (pension) ni musaada unaopewa kwa mstaafu ambaye hapati pensheni nyingine ya ziada ao ambaye kiasi cha pensheni yake ni kidogo. |
| **Äitiysraha**<br>Ätiysraha on etuus, jota äiti voi saada silloin, kun hän synnyttää lapsen. Maksu alkaa ennen lapsen syntymää (laskettua aikaa) ja sitä maksetaan noin 4 kuukauden ajan. | **Posho ya uzazi kwa mama**<br>Posho ya uzazi kwa mama ni pesa anayopewa mama wakati anazaa mtoto. Pesa hii inaanzakulipwa kabla mtoto hajazaliwa (muda uliohesabiwa) kwa kipindi karibuni cha myezi minne (4). |

| | |
|---|---|
| **Vanhempainraha**<br>Vanhempainraha on etuus, jota maksetaan vanhemmalle silloin, kun hän hoitaa pientä lasta kotona. Vanhempainrahaa voi saada äiti tai isä. Vanhempainrahaa voi saada noin puolen vuoden ajan. | **Posho ya wazazi**<br>Posho ya wazazi ni pesa anayopewa mzazi wakati anamchunga mtoto mchanga nyumbani. Posho ya wazazi anawezapewa baba ao mama. Posho ya wazazi hutolewa kwa muda wa myezi sita karibuni. |
| **Isyysraha**<br>Isyysraha on etuus, jota voidaan maksaa isälle, jotta hän voi hoitaa pientä lasta kotona. Isyysrahaa voi saada vain, jos isä asuu lapsen kanssa samassa kodissa. (Sinä aikana, kun isä saa isyysrahaa, hän voi hoitaa lasta osan ajasta yhdessä äidin kanssa ja osan ajasta yksin.) | **Posho ya uzazi kwa baba**<br>Posho ya uzazi kwa baba ni pesa ambayo inaweza kulipwa kwa baba ili aweze kumtunza mtoto mdogo nyumbani. Posho ya uzazi kwa baba inawezakutolewa kama baba anayeishi katika nyumba moja na mtoto. (Wakati baba anapopewa posho ya uzazi anaweza kumchunga mtoto pamoja na mama ao wakati mwingine peke yake). |
| **Kotihoidon tuki**<br>Kotihoidon tuki on etuus, jota maksetaan alle kolmevuotiaan lapsen hoitamisesta kotona. | **Posho ya malezi nyumbani**<br>Posho ya malezi nyumbani ni pesa inayolipwa kwa ajili ya kumtunza mtoto mwenye umri wa chini ya miaka 3 nyumbani. |
| **Elatustuki**<br>Jos vanhempi on yksinhuoltaja, eli yksin vastuussa lapsen elättämisestä, on hänellä oikeus saada rahallista tukea lapsen toiselta vanhemmalta. Jos toisella vanhemmalla ei ole varaa maksaa lapsen elättämisestä, voi yksinhuoltaja hakea rahallista tukea, eli elatustukea Kelasta. | **Mafao ya kumkimu mtoto**<br>Mafao ya kumkimu mtoto ni musaada. Ikiwa mzazi anamlea mtoto yeye mwenyewe basi ana haki ya kupewa musaada wa kifedha kutoka kwa mzazi mwenzake asiyeishi pamoja na wao. Na ikiwa mzazi huyu hana uwezo wa kulipia matunzo ya mtoto, anayemtunza mtoto anaweza kuomba mafao ya kumkimu mtoto kutoka Kela. |
| **Lapsilisä**<br>Lapsilisä on etuus, jota maksetaan jokaisesta Suomessa asuvasta lapsesta hänen huoltajalleen. Lapsilisä maksetaan siihen asti, kunnes lapsi täyttää 17 vuotta. | **Posho ya watoto**<br>Posho ya watoto ni msaada unaolipwa kwa kila mtoto anayeishi Finlande kwa mlezi wake. Posho ya watoto hulipwa hadi mtoto anafikia umri wa miaka 17. |
| **Yleinen asumistuki**<br>Yleinen asumistuki on etuus, joka on tarkoitettu vuokran maksuun. Asumistukea voit saada silloin, jos sinun tai ruokakuntasi tulot ovat pienet. Asumistuki ei koskaan ole niin suuri, että voisit maksaa sillä koko vuokran. | **Usaidizi wa kodi ya nyumba**<br>Usaidizi wa kodi ya nyumba ni musaada wa kifedha wa kulipia nyumba. Unawezapewa usaidizi wa kodi ya nyumba ikiwa kipato chako ao cha jamaa ni kidogo. Kawaida usaidizi wa kodi ya nyumba sio mwingi yaani hautoshi kulipia kodi (pesa ya nyumba) yote. |
| **Työmarkkinatuki**<br>Työmarkkinatuki on etuus, jota voidaan maksaa työttömälle. Usein työmarkkinatukea maksetaan, kun henkilö osallistuu koulutukseen, joka auttaa häntä pääsemään työhön. Suomeen pakolaisena tulleelle ihmisille Kela voi maksaa työmarkkinatukea, esimerkiksi silloin, kun hän osallistuu suomen kielen kurssille. Ennen kun voit hakea työmarkkinatukea Kelasta, sinun pitää ilmoittaa TE-toimistoon, eli Työ- ja elinkeinotoimistolle, että olet työtön. | **Mafao ya ukosefu wa kazi**<br>Mafao ya ukosefu wa kazi ni musaada ambao unaweza kulipwa kwa mtu asie na kazi au ajira. Mara nyingi mafao ya ukosefu wa kazi yanalipwa wakati mtu anashiriki kwenye mafunzo / masomo ambayo yatamsaidia kupata kazi / ajira. Kela inaweza kulipa mafao ya ukosefu wa kazi kwa mkimbizi ambaye amekuja Finlande kwa mfano, wakati anashiriki kwenye masomo ya lugha ya Kifini. Kabla ya kuomba mafao ya ukosefu wa kazi kutoka Kela, lazima kuijulisha Ofisi ya kazi na ajira kuwa hauna kazi / ajira. |

| | |
|---|---|
| **Ruokakunta**<br>Ruokakunta tarkoittaa yhtä henkilöä tai useampia henkilöitä, jotka asuvat samassa asunnossa. Esimerkiksi samassa asunnossa asuva perhe on yksi ruokakunta. Samassa ruokakunnassa olevien henkilöiden etuudet vaikuttavat toisiinsa. Jos asut ystäväsi kanssa samassa asunnossa ja teillä molemmilla on oma vuokrasopimus asuntoon, ette muodosta ruokakuntaa. | **Familia ya nyumba moja**<br>Familia ya nyumba moja inamaanisha mtu mmoja ao watu wengine wanaoishi katika nyumba moja. Kwa mfano jamaa linaloishi katika nyumba moja ni familia moja. Misaada ya watu wanaoishi katika familia moja inaathiriana moja kwa nyingine. Ikiwa unaishi na rafiki yako katika nyumba moja na kila mmoja wenu ana mkataba wa nyumba kivyake hapo hamuundi familia. |
| **TE-toimisto**<br>TE-toimisto on työ- ja elinkeinotoimisto. TE-toimistossa annetaan neuvontaa ja tarjotaan koulutusta silloin, jos olet työtön. TE-toimisto myös tutkii,voitko saada rahaa työttömyyden ajalta.Se antaa asiasta lausunnon, eli oman näkemyksen esimerkiksi Kelalle. Lausunnon perusteella Kela päättää, mitä etuutta työttämlle voi maksaa. | **Ofisi ya kazi na ajira (bureau ya TE)**<br>Ofisi ya kazi na ajira ni ofisi inayotowa ushauri na mafunzo kwa watu wasio na kazi na ajira. Ofisi ya kazi na ajira inachunguza pia ikiwa unaweza saidiwa kifedha kwa muda ule huna kazi. Ofisi hii hutowa taarifa na maoni yake kwa mfano kwa Kela. Kwa taarifa hiyo Kela inaamuwa ni aina gani ya musaada inapaswa apewe mtu asiyekuwa na kazi. |
| **Kulukorvaus**<br>Kulukorvaus on rahasumma, joka korvaa esimerkiksi matkakuluja. Kulukorvaus korvaa sellaisia matkakuluja, joita syntyy, kun työmarkkinatukea saava henkilö osallistuu koulutukseen. | **Fidia (récompense) ya matumizi ya ziada**<br>Fidia ya matumizi ya ziada ni kiwango cha pesa kinachofidia kwa mfano matumizi ya usafiri. Fidia ya matumizi ya ziada hufidia matumizi ya safari itokanayo na kuwa mtu anayepewa mafao ya ukosefu wa kazi na ajira anashiriki kwenye mafunzo (masomo). |
| **Kotoutumissuunnitelma**<br>Kotoutumissuunnitelma tehdään vasta maahan saapuneelle henkilölle. Suunnitelma tehdään TE-toimistossa, eli työ- ja elinkeinotoimistossa tai kotikunnassa. Kotoutumissuunnitelmassa sovitaan palveluista ja toimenpiteistä jotka edistävät niitä taitoja, joita sinä tarvitset suomalaisessa yhteiskunnassa. Kotoutumissuunnitelmassa voidaan sopia muun muassa osallistumisesta suomen kielen opiskeluun. | **Mpango wa kushirikishwa kijamii**<br>Mpango wa kushirikishwa kijamii hufanyiwa kwa mtu ambaye amefika siku za karibuni inchini Finlande. Mpango hufanyika kwenye ofisi ya kazi na ajira ( bureau ya TE) ao kwenye manispaa. Katika mpango wa kushirikishwa kijamii masikilizano yatafanyika kuhusu huduma na hatua zinazoweza kuhitajika ili upate ujuzi na uwezo wa kuishi vizuri katika jamii ya Finlande. Kwenye mpango wa kushirikishwa kijamii kunawezakuwa kusikilizana, pamoja na mambo mengine, kuhusu kushiriki kwenye masomo ya lugha ya Kifini. |
| **Perustoimeentulotuki**<br>Perustoimeentulotuki on rahallinen etuus, jota Kela maksaa. Sinä voi saada sitä silloin, kun sinun tai ruokakuntasi tulot tai etuudet eivät riitä välttämättömiin jokapäiväisiin menoihin, kuten asumiseen ja ruokaan. Perustoimeentulotuki on viimesijainen etuus. Toimeentulotukea varten tehdään aina laskelma ruokakunnan käytettävissä olevista rahoista. | **Posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi**<br>Posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi ni musaada wa kifedha kinacholipwa na Kela. Unaweza kuupata musaada huu ikiwa kipato na misaada vyako ao vya familia havitoshi kwa mahitaji muhimu ya kila siku kama vile kodi na chakula. Posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi huwa ni musaada wa mwisho kabisa unaoweza kutolewa. Maamuzi ya posho ya matumizi ya kimsingi huhesabiwa kutokana na pesa familia ilizonazo kwa matumizi. |
| **Täydentävä toimeentulotuki**<br>Täydentävä toimeentulotuki on etuus, jota voi hakea silloin, jos henkilöllä tai perheellä on pitkittynyt vaikea rahallinen tilanne. Täydentävää toimeentulotukea voi hakea joihinkin erityismeoihin, esimerkiksi pyykinpesukoneen ostoon silloin, jos talossa ei ole pyykkitupaa. Kunnan sosiaalityöntekijä arvioi, onko henkilöllä oikeus täydentävään toimeentulotukeen. | **Pesa ya matumizi ya ziada**<br>Posho ya matumizi ya ziada ni musaada ambao unaweza kuombwa kama mtu ao familia imekuwa katika matatizo ya kifedha kwa muda mrefu. Posho ya matumizi ya ziada inaweza kuombwa kwa matumizi yasiyokuwa ya kawaida. Matumizi yasiyokuwa ya kawaida yawezakuwa kwa mfano kununuwa mashini ya kufua kama katika jengo hakuna chumba cha kufulia. Mfanyakazi wa kijamii wa manispaa anaangalia ikiwa mtu ana haki ya kupewa pesa ya matumizi ya ziada. |

| | |
|---|---|
| **Ehkäisevä toimeentulotuki**<br>Ehkäisevä toimeentulotuki on etuus, jota henkilö voi hakea, kun hän on saanut päätösen perustoimeentulotuesta. Ehkäisevän toimeentulotuen tarkoituksena on ehkäistä henkilön tai perheen ongelmien kasvamista. Kunnan sosiaalityöntekijä tekee arvioi, onko henkilöllä oikeus ehkäisevään toimeentulotukeen. | **Posho ya kuepusha matatizo**<br>Posho ya kuepusha matatizo ni musaada ambao mtu anaweza kuomba, ikiwa kwenye uamuzi amekubaliwa posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi. Sababu za musaada wa kuepeusha matatizo ni kuzuia kuongezeka kwa matatizo ya mtu au ya familia. Mfanyakazi wa kijamii wa manispaa anaangalia ikiwa mtu ana haki ya kupatiwa musaada wa kuepusha matatizo. |
| **Toimeentulotukilaskelma**<br>Jotta oikeus perustoimeentulotukeen voidaan selvittää, Kela tekee laskelman hakijan (ruokakunnan) tuloista ja varoista, eli säästöistä ja omaisuudesta, sekä menoista. Kun ruokakunnan kaikki tulot on listattu, vähennetään niistä kaikki laissa määritetyt pakolliset perusmenot (asuminen, päivähoito, reseptilääkkeet, jne.). Tämän jälkeen hakijalle (ruokakunnalle) pitäisi jäädä laissa määrätyn summan, eli perusosan verran rahaa. Jos hakijalle (ruokakunnalle) ei jää tätä summaa, maksaa Kela perustoimeentulotukea niin paljon, että tämä summa täyttyy. Laskelma löytyy perustoimeentulotukipäätöksestä. | **Hesabu ya posho ya matumizi ya kimsingi**<br>Ili haki ya kupatiwa posho ya kwaida ya matumizi ya kimsingi iweze kufuatiliwa, Kela hufanya hesabu ya mapato na matumizi pamoja na mali na akiba (provision) kwa mwombaji (familia). Gharama zote za kimsingi zinazoelezwa na sheria (pesa za nyumba, malipo ya chekechea, gharama za madawa, nk) zitapunguzwa kutoka mapato ya familia yakishahesabika yote pamoja. Baada ya hayo mwombaji (familia) anapaswa kubaki na kiasi cha pesa kinachoelezwa kisheria, yaani sehemu ya msingi ya pesa. Ikiwa mwombaji (familia) hakubaki na kiasi hiki, analipwa posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi ili kiasi hiki cha pesa kieneye. Hesabu hupatikana kwenye maamuzi ya posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi. |
| **Perusosa**<br>Perusosa on toimeentulotukilaskelmassa käytetty termi. Sillä tarkoitetaan laissa määritettyä rahasumma, joka jokaisella tulisi jäädä kuukaudessa käyttöön perusmenojen maksamisen jälkeen. Perusmenoja ovat muun muassa asumiseen liittyvät menot, lääkärimaksut, reseptilääkkeet sekä päivähoitomaksut. | **Sehemu ya msingi**<br>Sehemu ya msingi ni neno ninalotumika katika mahesabu ya posho ya matumizi ya kimsingi. Inamaanisha kiwango kile cha pesa ambacho kisheria mtu inampasa abakiye nacho baada ya kulipa matumizi ya gharama za msingi. Matumizi ya gharama za msingi ni kwa mfano matumizi ynayohusika na makao, malipo ya daktari, pesa ya dawa na malipo ya chekechea (maternelle/jardin). |
| **Tiliote**<br>Tiliote on dokumentti, josta selviää oman pankkitilin rahatapahtumat. Tiliotteesta näkee paljonko tilillä on rahaa, mistä raha on tilille tullut ja mihin rahaa on käytetty. Tiliotteen saat omalta pankiltasi. Jos haet toimeentulotukea, sinun täytyy toimittaa hakemuksen liitteenä tiliote. | **Ripoti ya akaunti**<br>Ripoti / taarifa ya akaunti ni kibarua kinachoonyesha matumizi ya akaunti. Ripoti ya akaunti inaonyesha kiwango cha pesa kilichoko kwenye akaunti, pesa zilitoka wapi kuja kwenye akaunti na zimetumiwa namna gani. Taarifa hii unaipata kutoka benki yako. Unapoomba posho ya matumizi ya kimsingi lazima uambatanishe ripoti ya akaunti pamoja na ombi/fomu yako. |
| **Maksusitoumus**<br>Maksusitoumus on dokumentti, jonka avulla henkilö voi ostaa tietyn tuotteen tai palvelun. Maksusitoumuksen käyttäjä ei itse tällöin maksa myyjälle rahaa, vaan myyjä saa rahat maksusitoumuksen antajalta. Kela voi esimerkiksi antaa maksusitoumuksen silmälasien ostoa varten. Maksusitoumus voidaan antaa myös sähköisesti esimerkiksi lääkkeisiin. | **Hati ya ahadi ya malipo**<br>Hati ya ahadi ya malipo ni karatasi / baruwa inayoweza kutumiwa na mtu kwa kununuwa vitu ao huduma fulani. Mtumiaji wa hati ya ahadi halipi pesa kwa muuzaji (muuzishaji) bali muuzaji hupata pesa kutoka mtoaji wa hati ya malipo. Kela kwa mfano inawezapana hati ya malipo kwa ununuzi wa miwani (lunettes). Hati ya malipo inaweza kutolewa pia kielektroniki kwa ununuzi wa madawa. |

| | |
|---|---|
| **Kohtuulliset asumismenot**<br>Kela on määritellyt sen, mitkä ovat sopivan suuruisia eli kohtuullisia asumismenoja henkilölle, joka saa perustoimeentulotukea. Asumismenoja ovat esimerkiksi vuokra ja vesimaksu. Kohtuullisten asumismenojen suuruuteen vaikuttaa perheen koko ja kotikunta.<br><br>Jos vuokrasi on suurempi kuin Kelan määrittämät kohtuulliset asumismenot, Kela ei huomioi laskelmissaan kohtuullisen rajan ylittävää osaa vuokrastasi. Toisin sanoen, vaikka vuokrasi ylittää kohtuullisten asumismenojen rajan, saamasi etuuden määrä ei kasva. | **Matumizi ya kueleweka ya makao**<br>Kela imeamua kiasi cha gharama ya kodi kinachofaa kwa mtu anayepewa musaada wa posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi (posho ya kujikimu). Gharama za makao ni kwa mfano pesa ya kulipia kodi ya nyumba na ya kulipia maji. Kiasi cha matumizi ya kueleweka ya makao kinatokana na ukubwa wa familia na manispaa yenu.<br><br>Kela haitakubali katika mahesabu yao kiasi kinachozidi ile kodi ya nyumba inayokubaliwa na Kela. Kwa maneno mengine ikiwa kodi ya nyumba yako inazidi kiasi halisi kinachokubaliwa na Kela musaada unaopata hautaongezeka. |
| **Vuokran omavastuuosuus**<br>Vuokran omavastuu on se osuus vuokrasta, jota asumistuki ei korvaa. Henkilö maksaa itse tämän osan vuokrasta vuokranantajalleen.<br><br>Jos saat asumistuen lisäksi perustoimeentulotukea, voi Kela maksaa asumistuen ja perustoimeentulotuen suoraan vuokranantajan tilille, jos itse haluat niin. Mikäli asumistuki ja perustoimeentulotuki eivät yhdessä riitä koko vuokran maksamiseen, sinun täyty itse maksaa tililtäsi se summa vuokrasta, joka jää puuttumaan. Tämän summan maksamiseen voit käyttää palkkatulojasi, ja muita etuuksia, joita saat. | **Jukumu binafsi la kodi ya nyumba**<br>Jukumu binafsi la kodi ya nyumba ni sehemu ya pesa ya nyumba ambayo isiyolipwa kutoka usaidizi wa kodi ya nyumba. Mtu mwenyewe hujilipia sehemu hii kwa mpangishaji wake.<br><br>Kama pamoja na usaidizi wa kodi ya nyumba unapata posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi, Kela inaweza kulipa posho hizo moja kwa moja kwenye akaunti ya mpangishaji, ukitaka iwe hivyo. Endapo usaidizi wa kodi ya nyumba pamoja na posho ya kawaida ya matumizi ya kimsingi (ya kujikimu) hazitoshi kwa kulipa kodi yote ya nyumba, unapaswa kulipa kiasi kilichobaki kutoka akaunti yako. Kwa kulipa kiasi hiki unaweza kutumia mapato ya mshahara wako ao mafao / misaada mingine unayoipata. |
| **Palkka**<br>Palkka on rahasumma, jonka työnantaja maksaa työntekijälle tehdystä työstä. Palkka maksetaan tilille ja siitä vähennetään automaattisesti verot. Jos teet työtä ja saat palkkaa, ilmoita siitä Kelaan, sillä se vaikuttaa saamiisi etuuksiin. | **Mshahara**<br>Mshahara ni kiasi cha pesa ambacho muajiri (bosi) humlipa mfanyakazi kwa kazi aliyoifanya. Mshahara hulipwa kwenye akaunti na ushuru hukatwa moja kwa moja kutoka mshahara. Towa ripoti kwa Kela ikiwa unafanya kazi na kupokea mshahara kwani italeta mabadiliko kuhusu misaada unayopewa. |
| **Veronpalautus**<br>Suomessa melkein kaikista tuloista vähennetään automaattisesti jokin summa verona. Joka vuosi Verohallinto laskee, oletko maksanut veroa oikean määrän. Jos olet maksanut liikaa veroa, Verohallinto palauttaa ylimääräisen veron tilillesi. Veronpalautus vaikuttaa myös etuuksiin, esimerkiksi toimeentulotukeen. Jos saat paljon veronpalautusta, se voi vähentää toimeentulotuen määrää usean/monen kuukauden ajan. | **Marejesho ya ushuru (taxe)**<br>Inchini Finlande ushuru hukatwa moja kwa moja kutoka mapato ya kifedha karibu ya yote. Kila mwaka ofisi ya ushuru huhesabu ikiwa umelipa kiasi sahihi (kinachofaa) cha ushuru. Ikiwa umelipa zaidi, ofisi ya ushuru inakurudishia yale malipo ya ziada kwenye akaunti yako. Marejesho ya ushuru huleta mabadiliko kwa mfano katika utoaji wa musaada wa matumizi ya kimsingi. Ukirudishiwa pesa nyingi inaweza kupunguza kwa miezi kadhaa kiasi cha posho ya matumizi ya kimsingi. |
| **Tuen takaisinperintä**<br>Tuen takaisinperintä tarkoittaa sitä, että Kela pyytää takaisin maksamiaan etuuksia silloin, kun niitä on maksettu liikaa. Takaisinperintä voi tapahtua esimerkiksi silloin, jos perheesi asumisessa, työskentelyssä tai tuloissa on tapahtunut muutoksia, joista et ole ilmoittanut Kelaan. Muutokset perheessä vaikuttavat maksettavien etuuksien määriin. | **Ufilisi wa mafao**<br>Ufilisi wa mafao inamaanisha kwamba Kela inadai irudishiwe misaada, ikiwa imelipwa mingi kuliko. Ufilisi wa mafao unawezakutokea kwa mfano ikiwa katika ukaaji wa familia yako, katika kazi ao katika mapato kumekuwa mabadiliko, ambavyo havikujulishwa Kela. Mabadiliko katika familia yanabadilisha kiwango cha misaada inayotolewa. |

| | |
|---|---|
| **Eräpäivä**<br>Eräpäivä on laskun viimeinen maksupäivä. Jos et pysty maksamaan laskua viimeistään eräpäivänä, voit yrittää sopia uudesta eräpäivästä laskun lähettäjän kanssa. | **Tarehe ya mwisho ya malipo**<br>Tarehe ya mwisho ya malipo inamaanisha tarehe ya mwisho ya kulipa bili (facture). Unaweza kusikilizana naye anayekudai kuhusu tarehe mpya ya malipo ikiwa utashindwa kulipa bili hadi siku ya mwisho ya malipo. |
| **Maksumuistutus / maksukehoitus**<br>Maksumuistutus tai maksukehotus on laskun perijän lähettämä kirjallinen ilmoitus laskun maksajalle siitä, ettei laskua ole maksettu eräpäivään mennessä. Voit saada useampia muistutuksia silloin, jos et ole maksanut laskua. Jokainen muistutuskirjeen lähettäminen maksaa ja näin myös laskun kokonaissumma kasvaa. | **Kumbusho la kulipa bili**<br>Kumbusho la kulipa bili ni baruwa ya yule anayekudai kwamba hujalipa bili mbele ya tarehe ya mwisho. Unaweza kuzipata baruwa hizi nyingi ikiwa hujalipa bili. Kila kumbusho lina faini yake na hivi pesa za kulipa zinaongezeka kila kukija kumbosho. |
| **Maksuhäiriömerkintä / luottotietomerkintä**<br>Suomessa on koko maan laajuinen rekisteri, johon kirjataan maksuhäiriömerkintöjä. Maksuhäiriömerkintä syntyy, jos et maksa laskua muistutuksista huolimatta.  Maksuhäiriömerkintä voi tehdä elämästä vaikeaa, esimerkiksi asunnon tai puhelinliittymän saaminen voi olla vaikeaa. | **Kuondolewa uaminifu / ripoti ya kutokuaminika**<br>Inchini Finlande kuna rejista ya nchi nzima  kunakoandikwa ripoti za matatizo ya malipo. Ripoti ya matatizo ya malipo hutokea usipolipa bili hata baada ya kukumbushwa kulipa. Ripoti ya kutokuaminika inaweza kutatiza maisha na kuleta shida kwa mfano wakati wa kutafuta nyumba au laini ya simu ya kulipia kwa mwezi. |
| **Maksusuunnitelma**<br>Maksusuunnitelma tehdään silloin, jos on syntynyt velkaa, eikä velkaa voi maksaa kerralla kokonaan pois. Maksusuunnitelmassa sovitaan velkaa perivän osapuolen kanssa siitä, miten velka maksetaan takaisin osissa. Jos esimerkiksi Kela on maksanut sinulle liikaa etuutta, se perii liikaa maksetut etuudet takaisin. Jos et pysty kerralla maksamaan velkaa takaisin, voit sopia takaisin maksusta Kelan kanssa eli tehdä maksusuunnitelman Kelan kanssa. | **Mpango wa malipo**<br>Mpango wa malipo hufanyika wakati kumetokea madeni ambazo haziwezi kulipwa kwa mara moja tu. Mpango wa malipo ni makubaliano kati ya mdai na mdaiwa jinsi ya kulipa kwa nusunusu. Kwa mfano ikiwa Kela imekulipa pesa nyingi kuliko ilivyopaswa na inadai irejeshewe ziada hizo, unaweza kukubaliana na Kela kuhusu mpango wa malipo ya nusunusu. |

Rahoitus:

TURVAPAIKKA-, MAAHANMUUTTO- JA KOTOUTTAMISRAHASTO
Euroopan unionin tuella

Yhteistyössä:

Kela

Diak

IOM UN MIGRATION

TÚLKA

Suomen Pakolaisapu

Elinkeino-, liikenne- ja ympäristökeskus

Asumisneuvonta

Nurmijärvi

LOHJA Järvikaupunki

Sininauhasäätiö

www.sininauhasaatio.fi